Mwongozo Wa Mwanafunzi

2

# Kuitazama Biblia Kwa Haraka

## Kutambulisha neno la Mungu



MVMM

Mafunzo ya Vikundi Yanayohusu Maisha Mapya

# Kuitazama Biblia Kwa Haraka

## Kutambulisha neno la Mungu

Kimeandikwa Na David Batty

Mwongozo Wa Mwanafunzi

Toleo la Tano

MVMM
Mafunzo ya Vikundi
Yanayohusu Maisha Mapya

# Kuitazama Biblia Kwa Haraka

## Kutambulisha neno la Mungu

Kimeandikwa Na David Batty
Mwongozo Wa Mwanafunzi
Toleo la tano

Maandiko Yanayotumiwa Katika Kitabu Hiki Yametoka Kwa:

MAANDIKO: Biblia Takatifu (Union Version). Toleo La 1952, 1974, 1976, 1978. BST, BSK. Yametumiwa Kwa Ruhusa Maalum.

Tafsiri Ya Lugha Rahisi (TLR) itakayofanywa na mtafsiri ili kuleta maana halisi kama inavyosomeka katika lugha ya Kiingereza.

HakiMiliki © 2023, Teen Challenge USA.

Vitabu vya Mwalimu na kila kitu cha mwanafunzi vinavyohusiana na masomo haya ya *Mafunzo ya Vikundi Yanayohusu Maisha Mapya* vinanatawaliwa na Sheria za HakiMiliki. Mpango maalum umefanywa ili kufasiri masomo haya kwa lugha hii yaKiswahili. Masomo haya yanaweza kuchapwa na kugawanywa kwa ajili ya matumizi katika huduma za Teen Challenge na zinazofanana nazo, katika makanisa ya mahali pamoja, shule na mashirika mengine na hata watu binafsi. Pia, yanaweza kupatikana kutoka kwenye mtandao kwenye tovuti hii: www.iTeenChallenge.org Lakini, yasiuzwe. Yatolewe bure. Kwa wanaotaka kuchapisha na kuuza, wapate ruhusa kwa maandishi kutoka Global Teen Challenge.

Kwa mara ya kwanza, somo hili lilichapishwa kwa Kiingereza kwa jina lifuatalo:
*A Quick Look at the Bible, 5th edition*

Somo hili ni sehemu ya mfululizo wa masomo yaitwayo *Mafunzo ya Vikundi Yanayohusu Maisha Mapya* vinanatawaliwa ili kutumiwa makanisani, mashuleni, katika huduma gerezani, huduma za Changamoto Kwa Vijana, na huduma zingine kama hizo zinazofanya kazi na Wakristo Wapya. Vile vile kuna vifaa vingine vinavyopatikana kwa ajili ya mafunzo haya, kama kitabu cha kumwongoza mwalimu, cha kumwongoza mwanafunzi, kitabu cha kuongoza mafunzo cha mwanafunzi, mtihani, na cheti. Ukitaka habari zaidi juu ya masomo haya, wasiliana na:

Global Teen Challenge
PO Box 511
Columbus, GA, 31902 USA
Barua Pepe:gtc@globaltc.org
Tovuti: www.globaltc.org na
www.iTeenChallenge.org

MVMM
Mafunzo ya Vikundi
Yanayohusu Maisha Mapya

Mwaka wa Mwisho Kuhakikiwa: 02-2023

# Yaliyomo

Utangulizi ....................................................................................................4

**Sura ya 1. Habari za jumla kuhusu Biblia .....................................................5**

A. Kweli za msingi kuhusu Biblia...................................................................5

B. Umoja (au Kuunganika) wa Biblia.............................................................6

C. Kuipata picha nzima (au, ufunuo unaoendelea) ........................................6

D. Kristo anaingiaje katika Biblia nzima?......................................................6

E. Jinsi miaka inavyohesabiwa .......................................................................7

**Sura ya 2. Jinsi Biblia ilivyoandikwa..................................................................8**

A. Uvuvio – Nini maana yake? .......................................................................8

B. Mungu aliwavuviaje watu waandike vitabu vya Biblia? ...........................9

C. Jinsi Biblia ilivyotufikia sisi ....................................................................10

**Sura ya 3. Nawezaje kujua kwamba Biblia ni sahihi? .................................. 11**

A. Unabii wote ndani yake umekuwa wa kweli na sahihi kabisa .................11

B. Biblia inasema ni Neno la Mungu ............................................................11

C. Yesu alisema Biblia ni Neno la Mungu....................................................12

D. Katika Biblia hakuna kupingana...............................................................12

E. Akiolojia inathibitisha kwamba Biblia ni sahihi ......................................13

F. Taratibu za kimatibabu katika Biblia zinaithibitisha kwamba ni sahihi...13

G. Wewe mwenyewe jithibitishie kwamba Biblia ni ya kweli kwa kupima mafundisho yake katika maisha yako ........................14

**Sura ya 4. Kulitazama Agano la Kale kwa kifupi ...........................................15**

**Sura ya 5. Kulitazama Agano Jipya kwa kifupi .............................................17**

# Utangulizi

Leo kuna watu wengine wanaouliza hivi: “Kwa nini nisome Biblia? Imepitwa na wakati. Biblia iliandikwa miaka elfu mbili iliyopita. Itawezaje kunisaidia mimi leo, na matatizo niliyo nayo?”

Je, tunaweza kupata majibu ya maswali hayo?

Biblia inayo majibu ya maswali ambayo watu wanauliza leo, kuhusu maana na kusudi la maisha. Biblia inatuambia sisi ni nani, kusudi letu ni nini, chanzo cha matatizo yetu, na ufumbuzi wa matatizo hayo. Biblia ina maelekezo kuhusu njia kamilifu ya pekee kwa ajili ya kuishi.

Katika somo hili tutatazama Biblia nzima kwa haraka. Inahusu nini? Nani aliiandika? Ilifanyikaje mpaka ikatufikia sisi leo?

Kazi za mwanafunzi zipatikanazo katika *Mwongozo wa Somo* kwa ajili ya somo hili zimepangwa kukuingiza wewe katika Agano la Kale na Jipya ili ujionee mwenyewe vitabu hivyo vinahusu nini.

# Sura ya 1
# Habari za jumla kuhusu Biblia

## A. Kweli za msingi kuhusu Biblia

### 1. Kuna vitabu vingapi katika Biblia?

Vitabu 39 katika Agano la Kale
Vitabu 27 katika Agano Jipya
Katika Biblia nzima kuna vitabu 66

### 2. Ni watu wangapi walioandika hivyo vitabu 66 vilivyomo katika Biblia?

Watu wapatao 40 waliandika vitabu vya Biblia. Walitoka katika mazingira aina mbalimbali. Waandishi wengine walikuwa wakulima, wafalme, wavuvi, wamishenari, matabibu (madaktari), wahubiri, wafugaji, na maafisa wa serikali.

### 3. Ilichukua muda gani kuandika Biblia?

Biblia iliandikwa katika kipindi cha miaka kama elfu moja na mia tano hivi. Kitabu cha kwanza kuandikwa kilikuwa kitabu cha Ayubu. Hakuna tarehe ya uhakika inayotolewa kwamba kiliandikwa wakati gani, lakini pengine kiliandikwa wakati fulani kabla ya mwaka wa 1500 K.K. (Kabla ya Kristo). Kitabu cha mwisho kilichoandikwa kinaweza kuwa kitabu cha Ufunuo. Kiliandikwa wakati fulani kabla ya mwaka wa 100 B.K. (Baada ya Kristo). Vitabu vyote vya Agano Jipya vilikuwa vimeandikwa miaka isiyozidi 75 baada ya kufa na kufufuka kwa Yesu.

### 4. Je, Biblia hapo mwanzo iliandikwa kwa lugha zipi?

Agano la Kale liliandikwa kwa Kiebrania. Sehemu chache za Agano la Kale zilikuwa zimeandikwa kwa Kiaramu.

Agano Jipya liliandikwa kwa Kiyunani.

Agano la Kale liliandikwa kwa Kiebrania kwa sababu wakati vitabu hivyo vilipoandikwa, lugha iliyotumiwa na watu wote wa Israeli ilikuwa Kiebrania.

Wakati wa kuandikwa kwa vitabu vya Agano Jipya, Kiebrania hakikuwa lugha ya watu wote tena. Lugha iliyokuwa ya watu wote ilikuwa Kiyunani. Ndiyo sababu vitabu vya Agano Jipya viliandikwa kwa Kiyunani.

## B. Umoja (au Kuunganika) wa Biblia

Kitu kimoja kinachoshangaza kuhusu Biblia ni jinsi vitabu vyote sitini na sita vinavyounganika – yaliyomo katika kila kitabu "yanaungana." Umoja wa Biblia unaelezeka vizuri zaidi kwa kumtazama mwandishi – Mungu. Yeye ndiye aliongoza watu mbalimbali kuandika Biblia.

Vitabu vyote 66 ni kumbukumbu kamili ya ujumbe wa Mungu kwetu. Katika Biblia tunapata habari zinazotueleza jinsi ya kuwa Mkristo, na jinsi ya kuishi maisha ya Kikristo yenye mafanikio.

## C. Kuipata picha nzima (au, ufunuo unaoendelea)

Ukitaka kupata uelewa mzuri juu ya kinachofundishwa na Biblia, unahitaji kuipata picha nzima. Ni rahisi kubandua kipande cha mstari hapa au pale katika Biblia, na kuonyesha kwamba inaunga mkono mafundisho yoyote.

Kwa mfano: Zaburi 14:1 inasema, "Hakuna Mungu." Ila, mistari mingine mingi sana katika Biblia (kuanzia Mwanzo 1:1) inaonyeshe wazi wazi kabisa kwamba kuna Mungu.

Zaburi 14:1 haipingani na mistari mingine inayofundisha kwamba kuna Mungu. Tatizo letu ni kwamba hatuna habari kamili. Hatujapata mstari wote. Tunapousoma mstari mzima, tunapata maana tofauti kabisa. Zaburi 14:1 inasema, "Mpumbavu amesema moyoni mwake, 'Hakuna Mungu.' "

Ni lazima tuwe waangalifu kujua kila kitu kinachosemwa na Biblia kuhusu mada fulani kabla ya kufanya maamuzi ya mwisho. Ni muhimu kuona kila kitabu, kila sura, na kila mstari kulingana na Biblia nzima, kwamba vinahusianaje.

Biblia iliandikwa katika kipindi cha miaka elfu moja na mia tano hivi. Kadiri miaka ilivyoendelea kupita, Mungu alifunua habari zaidi juu Yake Mwenyewe na jinsi anavyotaka sisi tuishi. Kila kitabu katika Biblia kinaendelea kutueleza mengi zaidi kuhusu Mungu.

Mfumo huo unaweza kuonekana juu ya kila somo kuu linalozungumziwa na Biblia. Huu utaratibu wa kufunua maelezo zaidi kadiri muda unavyoendelea kupita hujulikana kama "ufunuo unaoendelea."

## D. Kristo anaingiaje katika Biblia nzima?

Yesu Kristo ndiye mhusika mkuu katika Biblia. Biblia nzima imejengwa juu ya maisha ya Kristo. Agano la Kale linatazama mbele kuhusu kuja kwa Yesu. Yeye ndiye atakayekuja kuleta uhuru toka dhambini (yaani, wokovu).

Vitabu vyote vya Agano Jipya viliandikwa baada ya Yesu kurudi mbinguni. Agano Jipya linaeleza juu ya maisha ya Yesu hapa duniani. Pia linatueleza jinsi ya kujitayarisha kwa ajili ya kurudi kwa Kristo mara ya pili.

Tukio la muhimu kuliko yote lililoandikwa katika Biblia ni ufufuo wa Yesu. Alikuja duniani, alikua na kuishi miongoni mwetu. Alitufundisha na Yeye binafsi alituonyesha jinsi ya kuishi maisha ya Kikristo. Kisha akafa ili kupata adhabu kwa ajili ya dhambi zetu. Lakini cha muhimu kuliko vyote ni kwamba, alifufuka kutoka kwa wafu. Tunayo nafasi ya kumtumikia Mungu aliye hai. Si mfu.

## E. Jinsi miaka inavyohesabiwa

Biblia ilipoandikwa, watu hawakuhesabu miaka kama tunavyofanya sisi leo. Nchi nyingi zilihesabu miaka yao kwa kuanzia kwenye utawala wa mfalme mpya. Njia nyingine ilimkuwa kuhesabu miaka kuanzia kwenye tukio kubwa.

Tunapata mfano wa hilo katika Agano la Kale, wakati Sulemani alipokuwa mfalme. Katika 1Wafalme 6:1, tunasoma hivi, “Ikawa katika mwaka wa mia nne na thamini baada ya wana wa Israeli kutoka nchi ya Misri, katika mwaka wa nne wa kutawala kwake Sulemani juu ya Israeli . . .” Huu mstari unaonyesha kwamba njia zote mbili za kuhesabu miaka zilitumiwa katika Israeli wakati huo. Kila nchi ilikuwa na njia yake ya kuhesabu miaka.

Huu mfumo wetu wa sasa wa kuhesabu miaka ulitengenezwa miaka mia kadhaa baada ya Yesu kuzaliwa. Mfumo huu wa kuhesabu miaka unatumiwa katika karibu kila nchi duniani siku hizi.

Mwaka wa 2004 unamaanisha kwamba ni miaka elfu mbili na nne tangu Kristo kuzaliwa. Miaka kabla ya kuzaliwa kwa Kristo inahesabiwa kwa kurudi nyuma. Kwa mfano: Malaki, ambacho ni kitabu cha mwisho cha Biblia, kiliandikwa kama mwaka wa 400 K.K., yaani, miaka 400 kabla ya kuzaliwa Kristo. Musa aliandika kitabu cha Mwanzo kama mwaka wa 1500 K.K., yaani, miaka elfu moja na mia tano kabla ya kuzaliwa kwa Kristo.

# Sura ya 2
# Jinsi Biblia ilivyoandikwa

## A. Uvuvio – Nini maana yake?

Tunaposema, “Biblia ***imevuviwa*** na Mungu” tunamaanisha nini? Tunawezaje kugawa kitu hicho mpaka kieleweke vizuri? Kuna mistari mitatu katika Biblia inayoshughulikia jambo hilo moja kwa moja. (2 Timotheo 3:16 na 2 Petro 1:20-21)

**2 Timotheo 3:16 BIBLIA Maandiko Matakatifu**

**“Kila andiko, lenye pumzi ya Mungu . . .”**

**2 Timotheo 3:16 BIBLIA Tafsiri Ya Neno**

**“Maandiko yote yamepuliziwa na Mungu . . .”**

**2 Timotheo 3:16 Tafsiri Ya Lugha Rahisi**

**“Maandiko yote matakatifu yametolewa na Mungu, na kuhuishwa Naye . . .”**

Mstari huu unatuonyesha kwamba maana ya “kuvuviwa na Mungu” ni kwamba:

1. Mungu alitupa Biblia.
2. Maandiko “yana pumzi ya Mungu” na “hutiwa uhai Naye.” Si maneno tu ambayo yamekufa, yaliyoko ndani ya kitabu. Unapolichukua Neno la Mungu na kulifanyia kazi maishani mwako, linatenda kazi! Neno la Mungu linakuwa hai, na Mungu anaanza kubadilisha maisha yako!

Tunaambiwa mambo mengine mawili katika 2 Petro 1:20-21, yanayotusaidia kuelewa maana ya kusema “Biblia imevuviwa na Mungu.”

**2 Petro 1:20-21 BIBLIA Maandiko Matakatifu**

**[20]Mkijua neno hili kwanza, ya kwamba hakuna unabii katika maandiko upatao kufasiriwa kama apendavyo mtu fulani tu. [21]Maana unabii haukuletwa popote kwa mapenzi ya mwanadamu; bali wanadamu walinena yaliyotoka kwa Mungu, wakiongozwa na Roho Mtakatifu.**

3. Hakuna sehemu yoyote ya Biblia iliyotungwa na mwanadamu.
4. Hao waandishi walinena (na kuandika) walichoambiwa na Roho Mtakatifu.

Tunaposema “Biblia imevuviwa na Mungu” tunamaanisha kwamba:

> **Roho Mtakatifu aliongoza mawazo ya waandishi kuandika yale Mungu aliyotaka waandike.**

Ni muhimu sana kuelewa kwamba Biblia yote nzima imevuviwa na Mungu. Vitabu vyote vimevuviwa na Mungu kwa kiwango sawa. Hakuna vitabu vingine “vilivyovuviwa zaidi” ya vingine.

## B. Mungu aliwavuviaje watu waandike vitabu vya Biblia?

### 1. Mungu hakuwaambia yale maneno ya kuandika (kwa sehemu kubwa)

Hawakuketi chini na kusikia sauti kubwa ikisema, “Huyu ni Bwana Mungu. Yafuatayo ndiyo yanayosemwa katika Isaya sura ya nne …” Yapo maeneo machache katika Biblia ambapo Mungu alimwambia mwandishi moja kwa moja maneno ya kusema. Mfano mmoja ni zile Amri Kumi.

### 2. Mungu hakuongoza mikono yao kuandika

Hawa waandishi hawakupigwa ganzi na Mungu kisha kuagizwa kuandika vitabu vya Biblia. Mungu hakuwafanya watu hao kuwa kama mashine. Walikuwa wanajua vizuri kile walichokuwa wanafanya.

### 3. Roho mtakatifu aliwapa mawazo ambayo wao waliyafafanua kwa namna yao wenyewe

Vitabu vya Biblia ni maneno ya Mungu yaliyoandikwa kwa mtindo wa waandishi.

Mungu alichagua watu wa aina mbalimbali kuandika vitabu vya Biblia. Kuna waliokuwa na elimu nzuri, na wengine hawakuwa na elimu. Mungu alimchukua kila mtu kama alivyokuwa na akamtumia kuandika kitabu kimoja au zaidi katika Biblia. Utakutana na mitindo aina mbalimbali ya uandishi katika vitabu vya Biblia. Kuna ambavyo vimeandikwa kwa urahisi sana. Vingine vimeandikwa kwa ugumu. Vingine vimeandikwa kiusomi kabisa.

Hawa watu waliandika kile ambacho Mungu alitaka waandike. Walimpenda Mungu na walikuwa wakifuata mafundisho Yake, lakini hawakuwa wakamilifu. Ila, ni vizuri tuamini kwamba Biblia ni ya kweli. Ni sahihi kabisa – haina makosa wala hitilafu. Kwa nini? Kwa sababu Mungu alikuwa anasimamia shughuli nzima, Naye hafanyi kazi kizembe. Biblia ni ujumbe wa Mungu kwa mwanadamu. Yote ni kweli, na NDIYO UKWELI. Katika maombi Yake katika Yohana sura ya 17, Yesu analiweka jambo hilo kwa uwazi kabisa.

**Yohana 17:17 Tafsiri Ya Lugha Rahisi**

**Wafanye kuwa watakatifu kwa ajili Yako Mwenyewe kwa kutumia ukweli. Neno Lako ni kweli.**

## C. Jinsi Biblia ilivyotufikia sisi

### 1. Vitabu vya kwanza viliandikwaje?

Karatasi tulizo nazo siku hizi hazikuwepo wakati vitabu vya Biblia vilipoandikwa kwa mara ya kwanza, miaka elfu nyingi iliyopita. Hivyo, watu walioandika vitabu vya Biblia waliviandika kwenye ngozi za wanyama zilizoshonwa na kuunganishwa pamoja vipande virefu, kisha vikakunjwa. Viliitwa magombo.

Hawakuwa na mitambo ya uchapishaji wala kompyuta wakati huo, hivyo, vitabu vyote viliandikwa kwa mkono.

Zile nakala halisi za vitabu vya Biblia hazipo leo. Lakini, kuna baadhi ambazo zina vitabu mbalimbali vya Biblia. Baadhi ya nakala hizo zilitengenezwa katika kipindi cha miaka mia moja tokea kitabu chenyewe kuandikwa.

### 2. Je, vitabu vya Biblia vilinakiliwaje?

Vitabu vya Biblia vyote vilikuwa vinanakiliwa kwa mkono. Katika nyakati za Agano la Kale, watu walikuwa na kazi ya kudumu ya kutengeneza nakala za Biblia. Sheria za kunakili vitabu hivyo zilikuwa kali sana. Makosa hayakuruhusiwa. Kama mtu angekosea, alitakiwa kutupilia mbali nakala aliyokuwa anaandika, na kuanza upya. Sheria hizi kali zilithibitisha kuwa za thamani sana, kwa sababu zilisaidia kudumisha usahihi wa Biblia katika miaka yote.

Nakala nyingi za vitabu vya Biblia zilizoandikwa kwa mkono bado zipo mpaka leo. Baadhi ya hizo ziliandaliwa miaka mia moja hadi mia mbili kabla ya kuzaliwa kwa Kristo. Hizo nakala za Biblia ni za thamani sana. Sehemu kubwa ya tafsiri za Kiswahili za Biblia zimetokana na magombo hayo ya Kiebrania na Kiyunani.

# Sura ya 3
# Nawezaje kujua kwamba Biblia ni sahihi (na ya kweli)?

Biblia iliandikwa miaka elfu mbili hadi elfu tatu iliyopita. Tunawezaje kujua kama Biblia ni sahihi? Tunawezaje kujua kwamba Biblia ni ya kweli? Tutajuaje kwamba Biblia haijabadilishwa? Labda imejaa makosa. Tutajuaje kama watu hawajaipotosha Biblia na kuibadilisha?

Zipo sehemu nyingi tunazoweza kutazama ili kupata ushahidi wenye nguvu kutufanya tutambue kwamba Biblia tuliyo nayo ni sahihi, haina makosa, na ni ya kweli. Tutakuwa na uhakika kwamba haijajaa makosa.

## A. Unabii wote ndani yake umekuwa wa kweli na sahihi kabisa

Neno “unabii” kwa kawaida lina maana mbili.

(1) Ni ujumbe kutoka kwa Mungu, unaotolewa na Mkristo.

(2) Ni utabiri – Ujumbe toka kwa Mungu, unaoeleza kitakachotokea wakati ujao.

Biblia imejaa mamia ya unabii. Kuanzia Mwanzo sura ya tatu hadi mwisho wa kitabu cha Ufunuo, Mungu ametupa sisi jumbe nyingi sana, na utabiri. Hakuna unabii hata mmoja uliokosewa. Unabii mwingi katika Biblia ulizungumza juu ya kuja kwa Yesu mara ya kwanza. Kila unabii ulitimizwa, kama Mungu alivyokuwa amesema. Isaya 53 na Zaburi 22 ni maandiko mawili yenye unabii kuhusu Yesu. Ona pia Mathayo 5:17-18, Yeremia 28:9, na Luka 21:24.

Bado kuna unabii mwingi ambao haujatimia. Sehemu kubwa hushughulikia kurudi kwa Yesu mara ya pili. Tunapotazama nyuma jinsi ambavyo ule unabii mwingine uliopita ulivyotimizwa, tunaweza kumwamini Mungu kabisa kwamba atatimiza unabii wote unaohusiana na kurudi kwa Yesu mara ya pili.

## B. Biblia inasema ni Neno la Mungu

Watu walioandika Biblia wanasema wazi kabisa kwamba ni Neno la Mungu. Mungu aliwaongoza wao na kuwaambia cha kuandika. Waandishi wanasema Mungu anahusika na kile walichoandika.

2 Timotheo 3:16
2 Petro 1:20-21

## C. Yesu alisema Biblia ni Neno la Mungu

Katika maisha Yake, Yesu mara kadhaa anatamka wazi wazi kwamba Biblia ni ya kweli, na kwamba ni Neno la Mungu. Yesu alionyesha imani Yake thabiti ya Biblia, kwa kutumia mafunzo ya Biblia kila siku katika maeneo yote ya maisha Yake.

Yohana 17:17
Yohana 10:35
Mathayo 5:17-18

Ikiwa Biblia si Neno la Mungu, na ikiwa Biblia si kweli, basi Yesu alidanganya katika Yohana 17:17. Kama Yesu alidanganya, maana yake ni kwamba alitenda dhambi. Ikiwa Yesu alitenda dhambi, basi kifo Chake pale msalabani hakiwezi kwa namna yoyote ile kulipia adhabu ya dhambi zetu. Lakini, hebu soma maandiko yafuatayo uone yanasema nini juu ya maisha ya Yesu.

Waebrania 4:15
Waebrania 5:8-9
1 Petro 3:18

## D. Katika Biblia hakuna kupingana

Kupingana ni kitu gani?

Ni wakati matamko mawili tofauti yanapodai yote kuwa ni ya kweli, na huku yote yako kinyume kabisa na kutofautiana kabisa. Maana yake ni kwamba, kama tamko moja ni la kweli, bali lile jingine lazima liwe la uongo. Kwa mfano: Matamko haya mawili yanapingana. “Mbwa amekufa” na “Mbwa yuko hai.” Ikiwa moja ni la kweli, basi lile jingine si la kweli. Haiwezekani matamko yote mawili kuwa kweli kwa wakati mmoja.

Biblia haijipingi. Haiwezi kusema mahali pamoja kwamba kitu fulani ni kweli, na mahali pengine iseme kitu tofauti ni kweli. Biblia haisemi mahali pamoja kwamba “Mungu amekufa” halafu mahali pengine iseme “Mungu yu hai.” Kuna wakati itaonekana kama kwamba kuna hali ya kupingana katika Biblia. Mara nyingi tatizo ni kwamba, mhusika anataja sehemu tu ya mstari, na haelewi ujumbe mzima wa mstari huo au sura hiyo.

Biblia ina umoja mkubwa sana. Biblia yote inatoa ujumbe mmoja tu uliounganika. Njia pekee ya hilo kufanyika ni kuwa mwandishi mmoja tu wa Biblia. Mungu ndiye mwandishi huyo. Yeye aliongoza kuandikwa kwa vitabu vyote 66 vya Biblia. Ndiyo sababu Biblia haina kupingana.

## E. Akiolojia inathibitisha kwamba Biblia ni sahihi

Elimu ya akiolojia inatoa ushahidi wa usahihi wa Biblia. Akiolojia ni nini? Kamusi moja imefafanua hivi: “Ni sayansi au mafunzo kuhusu maisha ya kale na historia, kwa njia ya kufukua au kuchimba na kupata miji iliyofukiwa, mahekalu, vifaa, na kadhalika.” (Tafsiri imetoka *The Courtis-Walter Illustrated Golden Dictionary for Young Readers*, Golden Press)

### 1. Wana Akiolojia wametumia miaka mingi sana kufukua na kujifunza juu ya miji ya kale iliyokuwepo wakati Biblia ilipoandikwa

Kuna vitabu mamia kwa mamia ambavyo vimeandikwa juu ya ugunduzi mbalimbali wa akiolojia. Hakuna kweli hata moja ya KiBiblia iliyothibitishwa kuwa ya uongo. Hakuna mwanaakiolojia hata mmoja aliyethibitisha kwamba Biblia imekosea katika habari inazotoa juu ya miji, wafalme, na desturi.

### 2. Magombo yaitwayo Dead Sea Scrolls yanathibitisha kwamba Biblia ni sahihi

Magombo yaitwayo The Dead Sea Scrolls ni moja kati ya ugunduzi muhimu sana wa kiakiolojia katika karne ya ishirini. Magombo hayo yaligunduliwa mwaka wa 1947 katika sehemu ambayo siku hizi ni nchi ya Israeli. Magombo hayo yana nakala (au sehemu) za vitabu vyote vya Agano la Kale isipokuwa kimoja tu. Mengi yalitayarishwa kiasi cha miaka 100 hadi 200 kabla ya kuzaliwa kwa Yesu. Hizo nakala za vitabu vya Agano la Kale zina umri wa miaka elfu moja zaidi kuliko nakala zingine zozote za Agano la kale zilizowahi kujulikana kuwepo.

Hayo magombo ya Dead Sea Scrolls yalipolinganishwa na Biblia yetu ya leo, hakuna tofauti yoyote yenye maana iliyopatikana. Magombo hayo ni ushahidi wenye nguvu sana, unaothibitisha kwamba Biblia yetu ya leo ni sahihi, tena inaaminika. Hayo magombo yanatupa sisi uthibitisho wenye nguvu, kwamba Biblia tuliyo nayo leo inasema kile kile kilichosemwa ilipoandikwa kwa mara ya kwanza.

## F. Taratibu za kimatibabu katika Biblia zinaithibitisha kwamba ni sahihi

Mafundisho ya kitabibu katika Biblia yamethibitishwa kuwa sahihi (tena mengine ni ya hivi karibuni tu) kulingana na ujuzi wa kitabibu ulioko leo.

Tabibu S. I. McMillen, aliandika kitabu kiitwacho, *None of These Diseases* (Spire Books). Humo, anazungumzia sheria nyingi za kitabibu katika Biblia, na kuonyesha jinsi ambavyo ziko sahihi kabisa zinapolinganishwa na taratibu za kimatibabu za kisasa.

## G. Wewe mwenyewe jithibitishie kwamba Biblia ni ya kweli kwa kupima mafundisho yake katika maisha yako

Kama mafundisho ya Biblia ni kweli, basi unapoanza kuyafanyia kazi katika maisha yako ya kila siku, utaona mabadiliko yakianza kutokea. Kama mafundisho ya Biblia si ya kweli, basi hakuna chochote kitakachotokea maishani mwako utakapoanza kuyafanyia kazi.

Ukweli ni kwamba watu wengi sana – mamilioni kwa mamilioni – wamefanya hivyo. Wamepima wenyewe binafsi mafundisho ya Biblia na kujithibitishia wenyewe kwamba ni ya kweli – kwamba yanafanya kazi. Hata katika Biblia, tunapata mifano mingi ya watu kuthibitisha katika maisha yao kwamba mafundisho ya Mungu ni ya kweli.

**Marko 16:20 Tafsiri Ya Lugha Rahisi**

**Wafuasi wakaondoka hapo na kuhubiri kila mahali. Bwana alitenda kazi pamoja nao. Bwana akaonyesha kwamba Neno la Mungu ni la kweli kwa matendo ya kipekee waliyowezeshwa kufanya.**

Hii inaweza kuwa njia ya kusisimua sana ya kuthibitisha usahihi wa Biblia, unapothibitisha maishani mwako mwenyewe kwamba mafundisho ya Biblia ni ya kweli.

Malaki 3:10
Wakolosai 1:5-6
Yohana 7:16-17

# Sura ya 4
# Kulitazama Agano la Kale kwa kifupi

Biblia imegawanywa katika sehemu mbili zijulikanazo kama agano. Agano ni makubaliano, ni mkataba. Biblia ni agano kati yetu na Mungu.

Agano la Kale lilitolewa kwa Wayahudi. Linashughulikia muda unaoanzia wakati wa kuumbwa kwa dunia hadi miaka kama mia nne hivi kabla ya kuzaliwa kwa Yesu. Linasimulia uhusiano wa Mungu na watu kabla ya kuja kwa Yesu. Sehemu tatu kwa nne za Biblia ni Agano la Kale. Liliandikwa hapo mwanzo kwa lugha ya Kiebrania. Kuna sehemu chache za Agano la Kale zilizoandikwa kwa lugha ya Kiaramu.

Katika Agano Jipya, Mungu anatuambia ni kwa nini tuna Agano la Kale.

**1 Wakorintho 10:11 TLR**

**Basi mambo hayo yaliwapata wao (watu katika Agano la Kale) kwa jinsi ya mifano, yakaandikwa ili kutuonya sisi tusifanye kama wao; tuyasome na kujifunza kutoka kwao katika hizi siku za mwisho, dunia inapoelekea mwisho wake.**

Kuna maandiko mengine mawili yanayotupa ujumbe dhahiri kabisa kwamba, Mungu anathamini sana kinachosemwa na Agano la Kale.

**2 Timotheo 3:16-17 TLR**

**Maandiko yote yana pumzi ya Mungu, nayo yanafaa kwa kufundisha, kukemea, kusahihisha na kuelekeza katika haki, (17) ili mtu wa Mungu apate uwezo kamili kwa ajili ya kila tendo njema.**

**Waebrania 4:12 TLR**

**Maana, chochote Mungu anachotuambia kimejaa nguvu hai: kina nguvu kuliko kisu kikali sana, na kinakata upesi na kuingia ndani kabisa ya mawazo yetu ya ndani na shauku tulizo nazo katika sehemu zake zote, na kutuweka wazi, tuonekane kama tulivyo.**

Ifuatayo hapo chini ni orodha ya vitabu na migao ya Agano la Kale.

# Sehemu Tano Za Agano La Kale

### Vitabu Vya Musa

Mwanzo
Kutoka
Walawi
Hesabu
Kumbukumbu la Torati

### Vitabu Vya Historia

Yoshua
Waamuzi
Ruthu
1 Samweli
2 Samweli
1 Wafalme
2 Wafalme
1 Nyakati
2 Nyakati
Ezra
Nehemia
Esta

### Vitabu Vya Mashairi

Ayubu
Zaburi
Mithali
Mhubiri
Wimbo Ulio Bora

### Manabii Wakuu

Isaya
Yeremia
Maombolezo
Ezekieli
Danieli

### Manabii Wadogo

Hosea
Yoeli
Amosi
Obadia
Yona
Mika
Nahumu
Habakuki
Sefania
Hagai
Zekaria
Malaki

# Sura ya 5
# Kulitazama Agano Jipya kwa kifupi

Vile vitabu ishirini na saba vya Agano Jipya vinasimulia habari za maisha ya Yesu, na mambo yaliyotokea baada ya Yeye kurudi mbinguni. Vitabu vingi vinasimulia habari za huduma ya wanafunzi wa Yesu, na Paulo.

Ifuatayo hapo chini ni orodha ya vitabu na migao ya Agano Jipya.

## Sehemu Tano Za Agano Jipya

**Injili**

Mathayo
Marko
Luka
Yohana

**Historia Ya Kanisa**

Matendo ya Mitume

**Barua Za Paulo**

Warumi
1 Wakorintho
2 Wakorintho
Wagalatia
Waefeso
Wafilipi
Wakolosai
1 Wathesalonike
2 Wathesalonike
1 Timotheo
2 Timotheo
Tito
Filemoni

**Barua Za Jumla**

Waebrania
Yakobo
1 Petro
2 Petro
1 Yohana
2 Yohana
3 Yohana
Yuda

**Kitabu Cha Unabii**

Ufunuo